# MTIHANI WA PAMOJA WA NYANDARUA MAGHARIBI

# KIDATO CHA NNE

# KISWAHILI

## MWONGOZO WA INSHA

1. Umeteuliwa kuwa miongoni mwa watakaohutubia wananci kuhusu hali ya usalama nchini Kenya.Andika hotuba utakayowasilisha siku hiyo kuhusu visababishi vya ukosefu wa usalama na upendekeze hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kukabiliana na hali hii

Sababu

- Siasa – vyama vya siasa
- uchochezi kutoka kwa viongozi
- Chuki na uhasama baina ya makabila
- Umaskini
- Ukosefu wa ajira
- Vikundi haramu vya vijana k.m mungiki, sungusungu MRC nk
- Ugaidi
- Dhuluma za kihistoria

(Zozote nne)

**<u>Mapendekezo</u>**

- Wachochezi kuchukuliwa hatua za kisheria
- Wananchi kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa kuishi pamoja kwa amani
- Serikali na washikadau kushirikiana ili kukabili tatizo la umaskini
- Kubuni nafasi za ajira kwa vijana
- Serikali kukabili vikundi haramu na ugaidi vilivyo

(Yoyote manne)

**1.**

**2. Utovu wa nidhamu shuleni umesababishwa na mabadiliko katika sekta ya elimu. Jadili.**

**<u>Kuunga mkono</u>**

- Kuongeza masomo kwenye mtaala.
- Kuondolewa kwa adhabu ya viboko.
- Kuwepo kwa elimu ya bure ambapo watoto hawawajibiki kwa wazazi wao kwa kuwalipia karo shuleni.

- Kuongezeka kwa vipindi vya kufundisha kwa walimu.
- Uchache wa walimu shuleni.
- Wanafunzi kupewa mamlaka ya kuchunguza walimu kuripoti.
- Wanafunzi kupewa mamlaka ya kuweka rekodi ya mahudhurio ya walimu ya vipindi.
- Wanafunzi kuruhusiwa kukaa katika bodi za usimamizi za shule na hivyo kujilinganisha na walimu.
- Kuwakubalia wanafunzi kuenda shuleni na vifaa meme; tarakilishi na simu.
- Kuruhusu wanafunzi waliopevuka kiumri kusoma pamoja na wanafunzi wa umri mdogo.

**Kupinga**

- Wazazi kutowajibikia malezi ya wana wao.
- Walimu kuzembea kazini.
- Wanafunzi kuiga mienendo hasi ya ugenini.
- Athari za mabadiliko ya kiteknolojia.
- Mabadiliko ya haraka ya kimaumbile

**Masharti**

- Hili ni swali la mjadala.
- Mtahiniwa aweze kushughulikia pande zote za mada.
- Mtahiniwa aunge mkono na kupinga mada.
- Mtahiniwa anaweza kuwa na idadi sawa ya hoja kote kuwili.
- Mtahiniwa atoe msimamo wake.

- Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja moja upande mmoja na nne upande mwingine.

3. **Samaki huanza kuoza kichwani.**

- Samaki anapoanza kuoza, kawaida huanzia kichwani.
- Methali hii huweza kutumiwa kupigia mfano jamii ambayo imeharibika au iliyozama katika uozo kwa kuwa viongozi wake wameharibika.
- Si lazima mtahiniwa aeleze maana bayana na maana batini ya methali hii.

4. **Tunga kisa kinachoanza kwa maneno: Tulipofika katika lango kuu, niling'amua kuwa huu ndio ungekuwa mwanzo wa ukurasa mpya wa maisha yangu.**

- Mtahiniwa aandike kisa kitakachoafikiana na mdokezo huu.
- Kisa kianze kwa mdokezo huu.
- Kisa kionyeshe mwanzo mpya wa maisha kama vile, mwanafunzi kujiunga na taasisi mpya ya elimu, mhalifu kuingia lango la jela, mtu kuingia mahali pa kazi baada ya kutokuwa na kazi kwa muda mrefu.
- Kwa vyovyote vile mtahiniwa aonyeshe mwanzo wa maisha mapya; mazuri au mabaya.